



## Mawaidha kwa wazazi kabla ya kufunguliwa tena kwa shule

---

Kila mtu yuko na hisia tofauti kuhusu kurudi tena shuleni. Baadhi ya wazazi na watoto wanaweza kuwa wanahisi furuha – wengine wanaweza kuhisi wasiwasi kiasi. Hiyo ni sawa. Kuwa na mtazamo mtulivu na chanya kunaweza kumshawishi na kumsaidia mtoto wako kujirekebisha na kuzoea. Wakumbushe kuwa kuzungumza kuhusu fikra na hisia zao na wengine kutasaidia.

Wakumbushe kuwa kuna mtu wa kutoa usaidizi kila wakati iwapo wanao wasiwasi kuhusu jambo fulani.

Pia ni muhimu kuwakumbusha kuhusu mambo mazuri yanayohusihwa na kurudi tena shuleni – kama vile kuungana na marafiki, kuwa na ratiba ya siku na kurudi tena kushiriki katika shughuli za shuleni.

Kuwa na ratiba zinazofaa kutamsaidia mtoto wako kujirekebisha na kuzoea baada ya kurudi tena shuleni. Mhimize ale lishe bora, afanye mazoezi, aungane na marafiki wake na kuwa na mazoea mazuri ya kulala.

Kazi nyingi zimefanywa ili kuhakikisha kuwa shule zetu zinaendelea kwa namna salama na endelevu.

Tumeshuhudia maendeleo mengi katika mapambano dhidi Covid-19. Mambo mengi katika jamii yamefunguliwa tena na mengi ya mambo tunayopenda sana kufanya, au tunayoyategemea, tunaweza sasa kuyafanya tena.

Mamlaka ya afya ya umma yamezingatia kwa umakini hatua ambazo zinahitaji kuwekwa katika mashule, ili kumweka kila mtu akiwa salama.

Wameridhika kuwa wakati masharti na ratiba zinafuatwa shuleni na kila mtu, tunalindwa vizuri zaidi kutokana na virusi hivi.

Kila mwanafunzi na mfanyakazi sasa anaombwa azingatie masharti na ratiba hizi ambazo ni lazima zifuatwe ili kumweka kila mtu salama. Shule zitawakumbusha wanafunzi kuhusu mambo haya, kwa kutumia matoleo ya video hii yanayofaa kiumri, na zana nyingine.

Kwanza kabisa, ni muhimu sana kwamba yeyote aliye na dalili za Covid-19, ikiwa ni pamoja na homa, kikohozi, upungufu wa pumzi au matatizo ya kupumua, au upotezaji au ubadilikaji wa hisia zake za harufu nakuonja asiende shuleni. Tafadhali fuata maelekezo ya HSE kuhusu kujitenga na uwasiliane na daktari wako. Hakikisha kuwa wanafunzi wanajua kuwa iwapo watajihisi kuumwa wakiwa shuleni wanafaa kumjulisha mwalimu mara moja.

Mazoea mazuri ya unawaji mikono na usafi yatakuwa muhimu kwa wanafunzi wote. Hakikisha kuwa mtoto wako anajua kutumia shashi au tishu kwa kufunika mdomo anapokohoa au kupiga chafya au kutumia kiwiko cha mkono anapokohoa au kupiga chafya.

Katika viwango vya shule ya msingi na elimu ya baada ya shule ya msingi, taratibu za kuweka umbali wa kimwili unafaa kufuatwa na kila mtu.

Katika shule ya msingi, watoto wadogo hawahitajiki kuweka umbali wa kimwili, lakini watapangwa katika vikundi vidogo wakiwa darasani.

Wakati wa kuchukuliwa na kurejeshwa unaweza kuwa na shughuli nyingi. Tafadhali hakikisha uwekaji wa umbali wa kimwili kwa kufuata maelekezo ya shule kuhusu nyakati za kuenda na mahali pa kuenda. Na hata ingawa inaweza kuwa ngumu, ni muhimu wazazi kutokusanyika katika malango ya shule ili kuzungumza na kujuana kabla na baada ya shule. Kudumisha umbali wa kimwili, kuvaa barakoa na kukosa kuzubaa shuleni kutasaidia kuweka shule ya mtoto wako kama imefunguliwa.

Wafanyakazi katika shule zote, na wanafunzi wa elimu ya baada ya shule ya msingi, wanahitajika kuvaa kitambaa cha kufunika uso

Mhimize mtoto wako kutembea au kupeleka baiskeli hadi shuleni iwapo itawezekana na ni salama kufanya hivyo.

Wanafunzi watatengewa kiti katika usafiri wa shule ambacho wanafaa kukaa na wanafunzi katika elimu ya baada ya shule ya msingi watahitajika kufunika nyuso zao wanaposubiri na wanapoingia ndani ya basi.

Shule zitawasiliana moja kwa moja na familia ili kuzikumbusha kuhusu taratibu zilizowekwa. Zungumza pamoja mkiwa nyumbani kuhusu mambo yanayotarajiwa mkirudi tena shuleni.

Walimu wanaelewa kuwa elimu ya wanafunzi inaweza kuwa iliathiriwa wakati wa nyakati za mafundisho na masomo ya mbali, na watahirikiana na wanafunzi ili kushughulikia athari zozote.

Kumbuka sisi sote tuko na jukumu la kufanya ili watoto wahudhuri shule kwa namna salama. Ni muhimu ufuata mawaidha ya afya ya umma ili kuweka mazingira ya shule yakiwa salama.

Kwa zaidi angalia [gov.ie/backtoschool](http://gov.ie/backtoschool)